



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE



Simu Na: +255 (026) 2740016
Nukushi: +255 026 2740103
BaruaPepe: ded@makete.go.tz
Tovuti: <http://www.maketedc.go.tz>

Kumb. Na. **MK/SPV/2024/01**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri Wilaya ya Makete,
4 Barabara ya Bomani,
59582 MAKETE, NJOMBE,
S.L.P 6, MAKETE
10 Disemba, 2024

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.
TANZANIA.

**YAH: OMBI LA KUSAJILI MRADI WA KIWANDA CHA UZALISHAJI UNGA WA
NGANO (MAKETE DISTRICT COUNCIL WHEAT FACTORY)**

Husika na mada tajwa hapo juu.

2. Halmashauri ya Wilaya ya Makete kupitia Kampuni yake ya Makete District Council (T) Company Limited inakusudia kuwekeza katika kiwanda cha kuzalisha unga wa ngano kitakachoitwa Makete District Council Wheat Factory.
3. Ili kufanikisha adhama hiyo; Mnamo tarehe 02 mwezi Disemba mwaka 2024, Kampuni ya Makete District Council (T) Company Limited iliazimia kusajili mradi wake wa kiwanda cha kuzalisha unga wa ngano katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ili kupata faida na nafuu mbalimbali za kiuwekezaji zinazopatikana mara baada ya kusajiliwa.
4. Hivyo basi; kwa barua hii ninawasilisha kwako ombi la kusajili mradi wa Makete District Council Wheat Factory katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).
5. Aidha; pamoja na barua hii, nimeambatanisha fomu ya maombi chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022 ikisomeka sambamba na kanuni ya 42 ya Kanuni za Uwekezaji Tanzania pamoja na nakala za nyaraka zote muhimu zinazohitajika kama zilivyotajwa chini ya aya namba 02 katika Fomu ya Maombi.
6. Ni matumaini yangu kuwa ombi letu litakubaliwa.
7. Wako katika Ujenzi wa Taifa.

WILLIAM M. MAKUFWE
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE.

MKURUGENZI MTENDAJI KW.
MAKETE